Johari za Kiswahili 13

EAF PAM
PL8704
.M2
U52

upisho wa malenga

hassani mwalimu mbega

EAST AFRICAN LITERATURE BUREAU

UPISHO WA MALENGA

Umeandikwa na
HASSANI MWALIMU MBEGA
USTADH–SHUARA

EAST AFRICAN LITERATURE BUREAU
KAMPALA NAIROBI DAR ES SALAAM

Utangulizi

NI WAJIBU wa mwandishi kujieleza mwanzo kabla ya maandishi yake yote yaliyomo, hasa kwa mtungaji mpya kama nilivyo mimi. Lakini sitajieleza katika kitabu hiki, sababu kitabu hiki ni vuo la utangulizi wa vitabu vilivyopangwa mfuulizo mmoja, na likavuliwa vuo hili ambalo ni sehemu ndogo ya tungo zangu.

Nimekusudia mfuulizo uwe wa vitabu vitatu au vinne ili iwe rahisi kwa wasomaji kuvipata, kuliko kufanya kitabu kimoja chenye bei kubwa ambacho kitakuwa na wanunuzi wachache kwa ajili ya ughali wake. Nimechagua kukiita kitabu hiki, "UPISHO WA MALENGA". Na kitabu cha pili ni, "UKUMBI WA USHAIRI", cha tatu ni "DAFINA YA UMALENGA". Muongozano wa vitabu hivi, kila kimoja kimechukuwa mambo kadha ya ushairi, kwani kusudio langu si kueneza mashairi yangu laa, kusudio hasa ni kuwafunulia watunzi utunzi ufaao na usiofaa.

Ingawa watunzi ni wengi sana sasa lakini mashairi mengi si mazuri ya sifa ya ushairi, kadhalika daraja zote za utunzi zimetupwa na kushikiliwa daraja moja tu. Pia lugha ya kishairi siyo itumiwayo na wengi wa watunzi wa leo. Jambo hilo ingawa halichunguzwi na washairi, labda kwa kutofahamu, lakini tuna hasara kubwa ambayo imeufanya ushairi wa Kiswahili wa sasa usiwe wa thamani, na umedharauliwa sana. Kwa hivyo, nimevifanya vitabu hivi vimuonyeshe mtunzi hatuwa za kuwepuka utungo usiyo thamani na kufikia wenye thamani. Kwa hivyo, habari ambazo zimepangwa tayari katika vitabu viwili vya nyuma, haingekuwa vizuri kuzichanguwa, isipokuwa msomaji ambaye ana mapenzi au mtunzi juu ya ushairi basi avipate kila viwapo tayari kuuzwa, ili aone

faida zilizomo ambazo sikufanya hivi kwa ajili ya kutaka sifa.

Bali minajili ya manufaa ya watunzi wa wasomi wa mashairi wafaidike, kwani kuwapa watu faida kwa ajili ya manufaa ya wote ni bora kuliko ulimwengu mzima kukusifu wewe mtu mmoja. Nina hakika isiyo shaka, kwamba iwapo watunzi wa mashairi watakubali kujitaabisha kama nilivyojitaabisha, basi sifa bora ni yao, kwani watairudisha thamani ya ushairi iliyo potea.

Hata hivyo, sijisemi kuwa ni bingwa kuliko wote ingawa huenda kusudio hili likatimu, lakini hata niweje, hakuna nchi iliyookolewa na shujaa mmoja pekee, basi kwa nini niwe na choyo cha kuyaficha niliyoyapata iwapo nilibahatika nayo!

HASSANI MWALIMU MBEGA

1. MAJI

Shairi hili niliwapa watu wa jarida la ZUKA, 1967.

1. Sitara usinihini, kwako ninalo litaka,
Najua toka zamani, mrembo usie shaka,
Hakika mwangu moyoni, hilo lanipa mashaka,
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

2. Maji yalo kisimani, watu wanapoyateka,
Aula pale bombani, kufunga na kufunguka,
Maji huwa hayaneni, hayana la kutamka,
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

3. Nambie yasema nini, maji yanapochemka?
Pale yawapo chunguni, unapo kuyateleka,
Maji, chungu, kijikoni, na huku moto wawaka,
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

4. Maji umbo'le laini, mtu hawezi yashika,
Hayana mfupa ndani, wala mwili kuzunguka,
Vipi yaweza baini, neno la kutamkika!
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

5. Niliyaona zamani, hakaa kuyapulika,
Hayasikia kwa ndani, yasema huku yacheka,
Haona ni kuu shani, au mijuza kutuka,
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

6. Sinambie kwa kudhani, dhana haina hakika,
Ewe swahiba mwandani, sinache nikasumbuka,
Lipekue kwa makini, na katwaa kuzishika,
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

